TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

WIZARA YA KILIMO

TANZANIAJAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MWONGOZO WA UUZAJI WA MALI ZA VYAMA VYA USHIRIKA


**IMEANDALIWA NA:**

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA,

S. L. P 201,

**DODOMA**



JUNI, 2024 TOLEO LA KWANZA

## YALIYOMO

DIBAJI ........ ii

SEHEMU YA KWANZA ........ 1

1.0 UTANGULIZI NA CHIMBUKO LA MWONGOZO ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Chimbuko la Mwongozo ........ 1

SEHEMU YA PILI ........ 3

2.0 MALENGO, WALENGWA WA MWONGOZO PAMOJA NA TARATIBU ZINAZOPASWA KUZINGATIWA KABLA YA KUUZWA KWA MALI ........ 3

2.1 Malengo ya Mwongozo ........ 3

2.2 Walengwa wa Mwongozo ........ 3

2.3 Taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na Chama cha Ushirika kabla ya kuuza Mali ........ 3

2.4 Hatua za kufuata wakati wa kuuza mali za chama cha ushirika; ........ 4

SEHEMU YA TATU ........ 6

3.0 MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UTOAJI WA VIBALI VYA UUZAJI WA MALI ZA VYAMA VYA USHIRIKA ........ 6

SEHEMU YA NNE ........ 7

4.0 UFAFANUZI WA JUMLA ........ 7

4.1 Taratibu za Utoaji Vibali ........ 7

4.2 Masuala yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kutoa kibali ........ 7

HITIMISHO ........ 8

**DIBAJI**

Katika uanzishwaji na ukuaji wake Vyama vya Ushirika nchini vimekuwa vikimiliki mali kwa mamlaka yanayotolewa na kifungu cha 35 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya mwaka 2013. Aidha, pamoja na Vyama hivyo kuwa na haki ya kumiliki mali, wakati mwingine katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwa Wanachama, Vyama hutaka kuuza mali vinazomiliki kutokana na uchakavu wa mali, ulipaji wa madeni au kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Kutokana na changamoto zinazojitokeza wakati wa uuzaji wa mali za Vyama vya Ushirika nchini, Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika imeandaa Mwongozo huu ambao umeainisha utaratibu utakaotumika katika uuzaji wa mali za Vyama vya Ushirika nchini.

Mwongozo huu, umelenga kufafanua taratibu za msingi za kufuatwa katika uuzaji wa mali za Vyama vya Ushirika. Taratibu hizo zinatakiwa kuzingatiwa na Vyama Vyote vya Ushirika vinavyohitaji kuuza mali zake ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza mara baada ya kuuzwa kwa mali hizo.

Dkt. Benson O. Ndiege
**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI NA CHIMBUKO LA MWONGOZO

### 1.1 Utangulizi

Historia ya Ushirika nchini inaanzia kabla ya Uhuru wa Tanganyika, ambapo jamii ilielimishwa kuhusu umuhimu na manufaa ya kuwa na Vyama vya Ushirika, ili waweze kujikwamua kiuchumi na kijamii. Jamii ilihamasika na ikapelekea kuanzishwa kwa Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali, kutegemeana na shughuli za kiuchumi na kijamii zinazoendeshwa na Vyama hivyo, pamoja na mahitaji ya jamii husika.

Vyama vya Ushirika vimekuwa vikimiliki Mali mbalimbali kama vile; Ardhi, Majengo, Magari na Mitambo, Samani, Hisa pamoja na mali nyinginezo kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya mwaka 2013.

Pamoja na Vyama vya Ushirika kuwa na uwezo wa kumiliki mali, Vyama hivi pia vinao uwezo wa kuuza mali vinazozimiliki, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya mwaka 2013 pamoja na Kanuni za Vyama vya Ushirika, 2015. Hivyo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa mwongozo, kwa ajili ya kutoa utaratibu utakaotumika katika uuzaji wa mali za Vyama vya Ushirika nchini.

### 1.2 Chimbuko la Mwongozo

Chimbuko la mwongozo huu ni kutokuwepo kwa utaratibu ulioainishwa kwenye Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika, kuhusiana na taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na Vyama vya Ushirika kuhusiana na uuzaji wa Mali za Vyama vya Ushirika nchini. Aidha, kutokana na kutokuwepo kwa utaratibu huo, kumesababisha uwepo wa changamoto na malalamiko kuhusiana na namna ambavyo baadhi ya Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika wanavyouza mali za Vyama pasipo kuzingatia bei halisi ya soko, thamani ya mali husika, pamoja na hitaji la Chama husika kumiliki mali hizo.

Hivyo basi, ili kuweka taratibu za msingi za uuzaji wa mali za Vyama vya Ushirika nchini, Mrajis wa Vyama vya Ushirika anatoa Mwongozo huu kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kanuni ya 81 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika, 2015.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MALENGO, WALENGWA WA MWONGOZO PAMOJA NA TARATIBU ZINAZOPASWA KUZINGATIWA KABLA YA KUUZWA KWA MALI

### 2.1 Malengo ya Mwongozo

Lengo kuu la Mwongozo huu ni kuweka utaratibu wa uuzaji wa mali katika Vyama vya Ushirika nchini.

### 2.2 Walengwa wa Mwongozo

Ili kuhakikisha kuwa utaratibu wa uuzaji wa Mali katika Vyama vya Ushirika unaimarika zaidi, Mwongozo huu utatumiwa na Vyama vya Ushirika na Wadau wengine, wanaotaka kununua mali zitakazouzwa na Vyama vya Ushirika.

### 2.3 Taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na Chama cha Ushirika kabla ya kuuza Mali

Chama chochote cha Ushirika pindi kinapohitaji kuuza mali zake/yake, kinapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Uwepo wa sababu zinazothibitisha umuhimu wa kuuzwa kwa mali husika.

ii. Uwepo wa Azimio la Mkutano Mkuu ulioridhia kuuzwa kwa mali husika.

iii. Uwepo wa nyaraka halisi (original documents) za umiliki wa mali inayotakiwa kuuzwa na Chama husika;

iv. Uwepo wa taarifa ya uthaminishaji wa Mali uliofanywa na mtaalamu anaetambulika kisheria; na

v. Uwepo wa Mpango wa matumizi ya fedha.

## 2.4 Hatua za kufuata wakati wa kuuza mali za chama cha ushirika;

### 2.4.1 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa

Chama cha Ushirika kinachokusudia kuuza mali zake kitatakiwa kufanya yafuatayo;-

- Kuainisha mali inayotarajiwa kuuzwa;
- Kuandaa nyaraka zote za umiliki wa mali hiyo na;
- kujiridhisha katika mamlaka husika juu ya umiliki wa mali hiyo.

### 2.4.2 Mkutano Mkuu

Baada ya kuridhika na sababu za kuuza mali, Bodi ya Chama itawasilisha katika Mkutano Mkuu nia yao ya kuuza mali ili kupata idhini sawa na matakwa ya Kanuni ya 76(1) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika, 2015.

### 2.4.3 Uthanimishaji wa Mali

Baada ya kupata idhini ya kuuza mali husika katika Mkutano Mkuu, Bodi ya Chama inapaswa kuthaminisha mali husika ili kupata thamani halisi kabla ya kuuza. Uthaminishaji wa mali ya Chama cha Ushirika utafanywa na Mthamini anayetambulika na Sheria za uthaninishaji.

### 2.4.4 Maombi ya kibali kwa Mrajis/Waziri mwenye dhamana ya Ushirika.

Baada ya kukamilisha taratibu za uthaninishaji na kupata idhini ya Mkutano Mkuu, Chama cha Ushirika kitaomba kibali cha kuuza mali husika kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika. Kwa mali isiyozidi thamani ya shilingi bilioni moja ( Tsh 1,000,000,000) kibali kitatolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika, na kwa mali inayozidi thamani inayozidi shilingi bilioni moja (Tsh 1,000,000,000/=) kibali kitatolewa na Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya Ushirika.

Aidha, maombi yote ya kibali cha kuuza mali ya Chama cha Ushirika yenye thamani inayozidi shilingi bilioni moja (Tsh 1,000,000,000) yatapitishwa kwa Mrajis

wa Vyama vya Ushirika kabla ya kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya Ushirika.

### 2.4.5 Uuzaji wa Mali

Baada ya kukamilisha hatua zote zilizotajwa hapo juu, Chama kitauza mali husika kwa njia itakayokuwa imeainishwa kwenye kibali cha kuuza mali hiyo.

### 2.4.6 Kuondoa mali katika vitabu vya Chama.

Baada ya mali kuuzwa, Chama kitatakiwa kufuta mali hiyo katika vitabu vyake na kuondoa nyaraka zote zinazohusiana na mali hilo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UTOAJI WA VIBALI VYA UUZAJI WA MALI ZA VYAMA VYA USHIRIKA

Wakati wa ushughulikia wa maombi ya vibali vya kuuza mali za Vyama vya Ushirika , Ofisi ya Mrajis wa Vya Vyama vya Ushirika itapaswa kuzingatia mambo yafuatayo, kabla na wakati wa utoaji wa vibali husika:-

i. Uhalali wa umiliki wa mali inayoombewa kibali cha kuuzwa (Vyeti/Hati na Mizania ya Chama);

ii. Uwepo wa ridhaa ya Wanachama wa Chama cha Ushirika na Bodi ya Uongozi, kinachoomba kibali (Muhtasari wa kikao cha Bodi na Mkutano Mkuu, wenye Agenda ya uuzaji wa Mali husika);

iii. Taarifa ya Uthaminishaji wa Mali inayoombewa kuuzwa (taarifa iwe ya uthamini uliofanyika ndani ya kipindi cha miezi 6 wakati kibali kinaombwa);

iv. Uthibitisho kutoka katika Chama kuwa Mali inayoombewa kibali haina mgogoro wowote au kuwekwa dhamana kwa ajili ya mkopo; na

v. Nyaraka nyingine yoyote ambayo Mrajis ataona inafaa, ili kujiridhisha.

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 UFAFANUZI WA JUMLA

### 4.1 Taratibu za Utoaji Vibali

Utaratibu wa utoaji wa Vibali vya Uuzaji wa Mali, utagawanywa katika makundi mawili ambayo ni; mali zitakazotolewa kibali na Mrajis wa Vyama vya Ushirika, na kundi la pili ni mali zitakazotolewa kibali na Waziri mwenye dhamana ya Ushirika kama inavyofafanuliwa hapa chini:-

i. Kwa Mali zote zenye thamani inayoishia Tsh. 1,000,000,000/=, vibali vyake vitatolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika, na

ii. Mali zote zenye thamani inayozidi Tsh. 1,000,000,000/=, vibali vyake vitalotewa na Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya Ushirika, baada ya kuwasilishwa kwake na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

### 4.2 Masuala yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kutoa kibali.

Utaratibu wote wa uuzaji wa mali ya Vyama vya Ushirika utazingatia mambo yafuatayo;-

i. Maombi yote ya vibali vya uuzaji wa Mali, yanapaswa kuwasilishwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika, yakiwa na barua ya maombi, taarifa za uthamini wa Mali na Mihutasari ya Vikao vya Bodi na Mikutano Mikuu, pamoja na taarifa nyingine ambazo zitaonekana kusaidia upatikanaji wa vibali husika;

ii. Njia za uuzaji wa Mali hizo, zitaainishwa katika kibali kitakachotolewa;

iii. Mali iliyopewa kibali cha kuuzwa, itauzwa kwa thamani isiyopungua ile iliyoainishwa katika taarifa ya uthamani wa Mali husika. Endapo thamani hiyo haitafikiwa, ni lazima kuombwa kwa kibali kwa aliyekitoa kuuza mali husika;

iv. Kibali kitakachotolewa kitakuwa cha muda wa mwaka mmoja pekee, na iwapo muda huo utaisha pasipo kuuzwa kwa mali husika, kibali husika kitapaswa kuombwa upya; na

v. Mwongozo huu utahusisha, Mali za Vyama vya Ushirika vinavyoomba kuuza Mali, wakati Vyama husika vikiwa vinafanya kazi. Kwa Vyama vya Ushirika vilivyofutwa, Wafilisi wataendelea na uuzaji wa Mali zake na kulipa madeni kama ilvyoelekezwa katika Mwongozo wa Ufilisi wa mwaka 2022, ulitolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

**HITIMISHO**

Vyama vyote vya Ushirika pamoja na Wadau wanaotaka kununua mali za Vyama wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika mwongozo huu na hatimaye kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa ili kuwa na Vyama imara vinavyozingatia sheria, kanuni na taratibu za kiushirika kwa maslahi mapana ya Vyama, Wanachama na Taifa kwa ujumla.

Aidha, Mwongozo huu utasomwa pamoja na Mwongozo wa manunuzi kwenye Vyama vya Ushirika toleo la Aprili, 2022, na ikiwa mwongozo huu utahitaji ufafanuzi Wadau wanaohusika watatakiwa kuwasiliana na Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.